# KCPE 2020 PRACTICE EXAMINATION

# MODEL PAPER 1 KISWAHILI

## Chagua jibu sahihi kujaza vihasho vilivyoachwa.

Hakimu ___1___ mshtakiwa asakwe na ___2___ mahakamani. Mshtakiwa alikuwa ameachiliwa kwa ___3___ ya shilingi laki moja. Alikuwa ameshtakiwa kwa kosa la ___4___.

Ilisemekana alikuwa amemwibia mwenzake kwa njia ya ___5___. Baada ya kusomewa mashtaka, ___6___ na kuamriwa apelekwe ___7___ au atoe kiwango cha pesa.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | aliagizwa | aliagiziwa | aliagiza | aliagizana |
| 2. | afike | afikie | afikishe | afikishwe |
| 3. | dhamana | faini | fidia | pesa |
| 4. | jinai | ugaidi | uhaini | ulevi |
| 5. | hila | uadilifu | hongo | utu |
| 6. | alikiri | alighairi | aliruka | alikata |
| 7. | jela | korokoro | rumande | polisi |

Ni jambo la ___8___ kwa mwanafunzi ___9___ na nidhamu, bidii na uwajibikaji iwapo angetaka kufanikiwa. Wanafunzi wanatakiwa ___10___ na wenzao ili kuongezeana maarifa ___11___ si kwa kupotoshana. Kamwe mwanafunzi yeyote yule, ___12___ nafsini mwake ___13___ anaweza kufanikiwa ___14___. ___15___ asiyejua upweke ni uvundo?

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 8. | muhimu | muhali | hiari | dharua |
| 9. | kua | kukuwa | kuwa | kutokua |
| 10. | kutangamana | kutengana | kutengemaa | kutangaa |
| 11. | na | wala | hata | ilhali |
| 12. | asiidanganye | asidanganye | asijidanganye | asimdanganye |
| 13. | kua | yakuwa | yakwamba | kwamba |
| 14. | peke yake | pekee yake | peke | upekee |
| 15. | Kwani | wepi | Ni nani | Mgani |

**Kutoka swali la 16 – 30 Chagua jibu kulingana na maagizo.**

16. Miaka kumi ni mwongo. Je, kipindi cha miaka mia moja ni nini?
    A. Milenia B. Laki C. Karne D. Korija

17. Kipindi kirefu cha jua kali huitwa ________.
    A. masika B. kiangazi
    C. kipupwe D. matlai

18. Chagua kielezi kati ya haya.
    Chebet aliadhibiwa vikali kwa kuzembea ____.
    A. zebea B. Chebet C. adhibiwa D. vikali

19. Akisami $3/7$ huitwaje?
    A. Subui tatu B. Theluthi saba
    C. Subui theluthi D. Tatu saba

20. Nitamwitaje mama wa mume wangu?
    A. Shangazi B. Mamkwe
    C. Mavyaa D. Shemeji

21. Eneo la bunge huongozwa na ___________.
    A. waziri B. mbunge C. chifu D. rais

22. Chagua kiashiria katika sentensi hii.
    Pangoni mle mna nyoka hatari.
    A. pangoni B. nyoka C. hatari D. mle

23. Humo ndani mlikuwa _______________.
    A. kweusi tititi B. mweusi tititi
    C. peusi tititi D. nyeusi totoro

24. Kamilisha methali: penye miti ___________.
    A. pana njia B. pana wajenzi
    C. hapana wajenzi D. hapakosi mvua

25. Kitenzi lia katika hali ya kutendesha kitakuwa
    A. liza B. lilisha C. lisha D. lialia

26. Baada ya maamkizi Lulu alijibu "binuru" ulikuwa wakati gani?
    A. Adhuhuri B. Asubuhi
    C. Mchana D. Usiku

27. Mwaniki ni mroho ina maana ___________.
    A. ni mlafi B. ana huruma
    C. ana bidii D. ni mzembe

28. Mshororo wa pili katika shairi huitwaje?
    A. Tadhinia B. Uwili
    C. Mleo D. Mloto

29. Ugonjwa wa kipindupindu pia huitwa ______.
    A. tauni B. kifaduro
    C. waba D. kichocho

30. Mtu anayetoa hotuba hadharani huitwa _____.
    A. mhutubu B. hatibu
    C. katibu D. mkutubi

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 – 40.**

Pamoja na kuwepo kwa Wizara ya Jinsia na nafasi kubwa ya kidemokrasia, mashirika ya kutetea haki za wanawake na za binadamu kwa ujumla zastahili kutumia uwezo wa sheria hii kikamilifu na kwa njia zote ili kuipa uzito unaostahili.

Ni muhimu sana visa vyote vya kidhuluma dhidi ya wanawake na watoto au hata dhidi ya wanaume vinaripotiwa mara moja.

Haitasaidia kuwa na sheria ambazo hazifuatwi eti kwa sababu visa hivi vya uvunjaji wa haki za kibinadamu haviripotiwi.

Tusiruhusu kuona visa hivi vikitendeka na tunyamaze. Hata ikiwa ni katika familia tusinyamaze. Tumesoma visa vingi katika magazeti na kusikia vingine katika vyombo vya habari kuhusu wazee wanaonyanyasa watoto wao wa kike kimapenzi.

Mara nyingine tunasoma kuhusu kina mama wanaojua kwamba mambo hayo yanafanyika lakini wanaamua kunyamaza ili kuficha aibu hiyo. Hili ni jambo la kusikitisha sana na halipaswi kuachwa kuendelea.

Pia kuna visa vingi vya watoto wa kike wa shule za msingi wanaonyanyaswa kimapenzi na walimu wao. Mara nyingi walimu wakuu huficha visa hivi kuokoa walimu wao wasifutwe kazi au kufikishwa mahakamani.

Chama cha KNUT tayari kimeshajitokeza kusema kuwa hakitatetea mwalimu yeyote atakayenaswa akimdhulumu mwanafunzi wake kimapenzi.

Sasa muhimu ni kuhakikisha kuwa visa hivi vinamalizwa kabisa katika shule zetu na hata nyumbani.

Hata wanawake wengine ambao hutumia watoto wadogo wa kike katika biashara ya umalaya wanapaswa kukomeshwa mara moja. Vilabu vya usiku vinavyowaruhusu watoto wadogo au hata kuwauzia pombe vinapaswa kunyimwa leseni na pia kulazimishwa kufunga.

Hizi juhudi zinazopaswa kufanywa na watu wote wakiwemo polisi wa utawala, machifu na wazazi wote kwa pamoja.

Ni katika kushirikiana hivi ndipo tutaweza kupunguza visa hivi vya ugandamizaji wa watoto wa kike.

Bi Njoki Ndung'u anastahili pongezi kwa juhudi zake kubwa za kupambana na unyanyasaji huu kisheria. Anapaswa kuungwa mkono na Wakenya wote wenye nia njema.

31. Wizara za humu nchini huongozwa na _________.
    A. rais
    B. wabunge
    C. waziri
    D. katibu mkuu

32. Ni visa vipi vinakisiwa kutoripotiwa pindi tu vitokeapo?
    A. Dhuluma ya watoto wa kike na baba zao au walimu.
    B. Vita vya wanawake mitaani
    C. Unyanyasaji wa mwalimu mkuu
    D. Unywaji wa pombe kwa watoto wadogo

33. "Haitasaidia kuwa na sheria ambazo hazifuatwi" ina maana _________________________.
    A. sheria zitatufuata
    B. ni bure bilashi kuwa nazo
    C. hata zikifuatwa hazitasaidia
    D. heri kuunda nyingine

34. Ni jukumu la nani kuripoti visa vya dhuluma vitokeapo?
    A. Watoto
    B. Wanawake
    C. Wanaume
    D. Kila mzalendo

35. Neno <u>mara nyingi</u> limetumika. Kisawe chake ni
    A. aghalabu
    B. mighairi ya
    C. maadamu
    D. yakini

36. Kando na mwalimu kula kalenda aweza pia __________________.
    A. kupigwa kitutu
    B. kupigwa kalamu
    C. kutetewa
    D. kufichwa asionekane

37. Katika makala haya ni akina nani walio katika hatari zaidi?
    A. Walimu
    B. Wanawake
    C. Watoto wa kike
    D. Wazee

38. Wakenya wenye nia njema ni wepi?
    A. Wanaojua sheria
    B. Wauza pombe
    C. Wazalendo
    D. Wakenya wote

39. Kuunga mtu mkono ni kinyume na ______________.
    A. kukubaliana
    B. kupinga
    C. kushirikiana
    D. kupongeza

40. Mada mwafaka ya makala haya yaweza kuwa;
    A. udemokrasia
    B. wizara ya jinsia
    C. haki za watoto
    D. dhuluma za kimapenzi

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu kisahihi maswali 41 – 50**

"Leo ni siku ya kusema. Tena niacheni niseme nipendavyo kwani nimejawa na furaha isiyo na kifani.

Kwa miaka na dahari nilikuwa nikitamani ifike siku hii kabla sijaiaga Dunia. Nimejitolea kwa mapana na marefu, kwa hali na mali, ili tuweze kupata ushindi huu. Leo si ndoto tena bali ni ukweli mtupu. Kweli "Mtaka cha mvunguni ..........."

Ushindi huu si wangu peke yangu na wala nisingeweza kuupata bila ya msaada wa mkufunzi wetu, Bwana Ratiba, pamoja na wahusika wengine hasa nyinyi wachezaji. Yote ni kuthibitisha kwamba mkono mmoja haupigi kofi.

Wanasoka nyinyi hamkulinyanyua jina la mji wetu tu bali hata nchi nzima. Iwapo furaha yangu mimi iko hivi, je, yenu ikoje?

Zawadi nitakayowazadia sitaitaja sasa kwani wako wafadhili wengine ambao na wao wangetaka kutabaruku. Lakini itoshe kuwafahamisha kuwa kila mmoja wenu atapewa thuluthi mbili nyongeza ya mshahara wake ili kuwahamasisha mzidi kufanya vyema.

41. Katika kukamilisha methali angesema, "Mtaka cha mvunguni ____________________.
    A. anyanyue kitanda
    B. aondoe godoro
    C. asiogope kuumwa
    D. sharti ainame

42. Hotuba ilihutubiwa akina nani?
    A. Mashabiki
    B. Wakufunzi
    C. Washangiliaji
    D. Wachezaji

43. Bwana Ratiba ni ______________________.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748

E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

A. shabiki
B. msaidizi
C. msimamizi
D. mkufunzi

44. Aliposema, "Mkono mmoja haupigi kofi" alimaanisha _______________.
A. kofi hupigwa kwa mikoni miwili
B. Kufaulu kunahitaji kusaidiana
C. Kufaulu kwahitaji watu wawili.
D. Watu wawili wakisaidiana watafaulu

45. Kuhusu zawadi, anayeongea _______________.
A. aliitaja
B. hakuitaja
C. aliitoa
D. aliigawa

46. Kutabaruku ni _______________.
A. kutoa baraka
B. kubarikiwa
C. kujitolea
D. kuwaombea

47. Thuluthi mbili katika akisami ni _______________.
A. $3/2$
B. $1/3$
C. $2/3$
D. $30/2$

48. Lengo la kuwapa kiwango zaidi cha mshahara ni _______________.
A. kuwashukuru kwa kutimiza ndoto yake
B. kuwatia moyo wa kushindana
C. kuonyesha ukarimu wake
D. kuwafurahisha wasikilizaji wake

49. Kichwa kifaacho hotuba hii ni _______________.
A. usipoziba ufa
B. asiyekubali kushindwa
C. mwanzo wa ngoma
D. chanda chema huvikwa pete

50. Mwenye kuhutubu ni mtu _______________.
A. anayependa kujisifu
B. anayependa kuwatumia wengine
C. wa maneno bila vitendo
D. anayependa ushirikiano wa watu

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com